

## KILIMO BORA CHA KUNDE



**Lima kunde kwa lishe nkipato zaidi**

### 1. UTANGULIZI

Kunde ni zao jamii ya mikunde. Faida kubwa ya zao hili ni:

- Chanzo cha viini lishe vya protini kwa binadamu na wanyama.
- Mabaki ya mmea wa kunde ni chakula kizuri cha mifugo.
- Hurutubisha udongo.

### 2. AINA ZA KUNDE

Kunde za muda mrefu

**Tumaini** - Hutambaa na kuchukua muda wa siku 75-85 kukomaa

**Fahari**- Hutambaa na huchukua muda wa siku 90 kukomaa.

**Raha 1**- Haitambai na huchukua muda wa siku 74-80 kukomaa

**Raha 1**- Haitambai na huchukua muda wa siku 70-75 kukomaa.

### **Kunde za muda mfupi**

**Vuli-1 :** Hutambaa na kuchukua muda wa siku 75-85 kukomaa .Hutambaa na huchukua muda wa siku 90 kukomaa.

**Vuli-2 :**Haitambai na huchukua muda wa siku 74-80 kukomaa.Haitambai na huchukua muda wa siku 70-75 kukomaa

### **3. WAKATI WA KUPANDA**

- Sehemu zenyе misimu miwili ya mvua, kunde za muda mrefu zipandwe wakati wa masika (miezi miwili na nusu kabla ya kumalizika mvua).
- Kunde za muda mfupi zipandwe wakati wa wavuli, ili kumwezesha mkulima kupanda zao la aina nyingine kama mtama, mahindi au pamba katika shamba hilo wakati wa masika.
- Sehemu zenyе msimu mmoja wa mvua kunde za muda mfupi zipandwe miezi miwili kabla ya kumalizika kwa mvua.

### **4. NAFASI YA KUPANDA**

- Kunde zinazotambaa zipandwe kwenye nafasi ya sentimita 75 mstari hadi mstari na sentimita 20 shina hadi shina kwa kuweka mbegu mbili katika shimo. Wiki moja baada ya kuota punguza ubaki mche mmoja kila shimo.
- Kunde zisizotambaa zipandwe kwenye nafasi ya sentimita 50 mstari hadi mstari, na sentimita 20 shina hadi shina kwa kuweka mbegu tatu kila shimo. Wiki moja baada ya kuota punguzia ibaki miche miwili kila shimo

### **5.PALIZI**

Kwa matokeo mazuri, palilia kunde wiki baada ya kupanda.

### **6. KUZUIA WADUDU**

Ili kupata mavuno mengi kuzuia wadudu waharibifu kwa kupulizia dawa utakazo shauriwa na mtaalamu wa kilimo.

- Kwa kunde za muda mrefu, pulizia dawa mara tatu kuanzia wakati wa kutoa maua halafu kila bada ya siku kumi. Kwa kunde za muda mfupi, pulizia dawa mara mbili (baada ya kutoa maua na siku kumi baadaye).
- Kuna misimu ambapo wadudu wanaokula majani waitwao Vifurunzi au Vikombe hutokea kwa wingi. Wadudu hawa hutokea mara baada ya mimea kuota na wakitokea kwa wingi wanawenza kuleta hasara kubwa. Ili kuzuia wadudu hawa, weka dawa aina ya “Marshal” kwenye mbegu kabla yakupanda.



**Unyunyiziaji wa dawa kuua wadudu wanaoshambulia kunde shambani**

## 7. JINSI YA KUVUNA NA KUIADHI KUNDE

Kunde zivunwe wakati zimekauka vizuri. Vuna kwa kuchuma vitumba au kung’oa mashina kama vitumba vyote vimekauka umba vyote vimekauka.

- Anika kunde zilizovunwa juani kisha piga na fito, peta anika juani zikauke vizuri kisha hifadhi ghalani. Kunde hubunguliwaharaka, kwahiyo hifadhi ndani ya mifuko maalaum (PICS bags).

## 8. KIASI CHA MAVUNO

Kunde za muda mrefu zinaweza wa kutoa magunia 6 hadi 8 kwa ekari moja au kilo moja, 500-2,500 kwa hekta, na zile za muda mfupi magunia 6 hadi 7 kwa ekari au kilo 1,200 -2,000 kwa hekta kulingana na matunzo

Imepakuliwa :- 10/09/2024

Inapatikana :- <https://www.n2africa.org/sites/default/files/Cowpea%20Brochure%20Tanzania.pdf>